**13 NOVEMBA, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

**Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Novemba, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU NA TAMKO LA AHADI YA UZALENDO**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar.

*(Mbunge Aliyetajwa Hapo Juu Aliapa Kiapo cha Uaminifu na Tamko la Ahadi ya Uzalendo)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunasubiri hatua yetu ya pili, uthibitisho wa Waziri Mkuu. Ninamwomba Katibu asome maelezo mawili matatu kuhusu namna utaratibu utakavyokuwa. Karibu Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kumthibitisha Waziri Mkuu Bungeni ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Kiapo cha Uaminifu kwa Mbunge, Spika atapokea Hati ya Uteuzi wa Waziri Mkuu kutoka kwa Rais, baadaye Spika atalijulisha Bunge juu ya kupokea Hati ya Rais kuhusu uteuzi wa Waziri Mkuu ili athibitishwe na Bunge. Spika atafungua bahasha yenye hati hiyo mbele ya Bunge na kusoma mbele ya Bunge jina lililopendekezwa na Rais na kutaka Bunge kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa, tuna zoezi zito sana, ninaomba mtulie.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Spika anaweza kusitisha shughuli za Bunge ili kutoa nafasi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuandaa azimio la kumthibitisha Waziri Mkuu na Katibu wa Bunge kuandaa karatasi za kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge kurejea, Spika atamwita Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili atoe hoja kwa kuwasilisha Azimio la Kumthibitisha Waziri Mkuu Mteule kwa mujibu wa Ibara ya 52(2) ya Katiba. Katika maelezo yake anaweza kuelezea mamlaka na wajibu wa Waziri Mkuu kama ilivyoainishwa kwenye Ibara ya 52(1), (2) na (3) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo hatutengui Kanuni za Bunge kwa sababu anayeleta hati hiyo ni Mwanajeshi na ni Askari, na wao wana fursa ya kuingia ndani kwa mujibu wa Kanuni zetu. *(Makofi)*

Ninamwomba mhusika *ADC* aingie ndani. *(Makofi)*

*(Hapa Mpambe wa Rais aliingia ndani ya Ukumbi wa Bunge kukabidhi Jina la Waziri Mkuu Mteule)*

**BRIGEDIA JENERALI NYAMBURI MASHAURI - MPAMBE WA RAIS:** Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mimi ni Brigedia Jenerali Nyamburi Mashauri, Mpambe na Msaidizi wa Masuala ya Kijeshi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimeelekezwa na Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwasilisha ujumbe maalum kwako. Kwa heshima na taadhima ninaomba nikukabidhi. *(Makofi)*

*(Hapa Mpambe wa Rais alimkabidhi Spika bahasha iliyokuwa na Jina la Waziri Mkuu Mteule ili litangazwe Bungeni)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, "Uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 51(2), Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kushika madaraka yake ndani ya siku 14 atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka katika jimbo la uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, au kama hakuna chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi, basi atateuliwa anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata Hivyo, Waziri Mkuu atakayeteuliwa hatashika madaraka hayo hadi uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

Hivyo, kwa kutekeleza matakwa hayo ya kikatiba nimemteua Mheshimiwa... *(Kelele/Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba..." *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa ninaomba tukae, hajaapishwa bado. Sasa ninamruhusu mwakilishi wa

Mheshimiwa Rais aweze kurudi kwenye majukumu mengine. Ahsante sana Kamanda. *(Makofi)*

*(Hapa Mpambe wa Rais Aliondoka ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** "Hivyo, kwa kutekeleza matakwa hayo kikatiba nimemteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge, ili uteuzi wake uthibitishwe na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninakutakia majukumu mema, Mungu ibariki Tanzania. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile jina hili likija hapa ni siri, nasitisha Bunge kwa nusu saa ili Katibu akaandae *ballot paper*. *(Makofi)*

*(Saa 3.08 Asubuhi Bunge lilisitishwa kwa dakika 30 ili kukamilisha maandalizi ya karatasi za kupigia kura)*

*(Bunge Lilirejea)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA S. JOHARI - MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, naomba kuwasilisha maelezo kuhusu Hoja ya Serikali ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 ili niwasilishe Hoja ya Serikali kuomba Bunge lako Tukufu limthibitishe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyeteuliwa na Mheshimiwa Daktari Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatekeleza jukumu hili la kikatiba, naomba nianze kwa kumshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na karama mbalimbali, hivyo kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi kama tunavyomwomba kila siku ya shughuli za Bunge, ambapo pamoja na mambo mengine, katika dua yetu tunamwomba Mwenyezi Mungu aibariki nchi yetu idumishe uhuru, umoja, haki na amani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 62 na 63 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Bunge letu lina sehemu mbili, yaani sisi Wabunge ni sehemu ya kwanza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni sehemu ya pili. Mchakato wa demokrasia umeamua kwa dhahiri kabisa kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni chaguo la walio wengi katika nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo basi, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati kwa kuchaguliwa kwake kwa kura nyingi za kishindo kuiongoza nchi yetu kwa kipindi kijacho cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yeye, nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi aliyechaguliwa kwa tiketi moja na Mheshimiwa Rais kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, ambaye wananchi wa Zanzibar wamemchagua kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wametamka kwa kura zao na wameonyesha imani yao kubwa kwa viongozi wao kwamba wataendeleza mafanikio ya kiuchumi na kijamii yaliyokwishapatikana. Wataendeleza mazingira ya amani na utulivu na pia watadumisha Muungano wetu, umoja wa wananchi wetu na mshikamano baina ya wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua tena katika nafasi hii ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka zake na ninamwomba anipe busara, afya njema na ustahimilivu ili niweze kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba na kisheria na kuzingatia katiba na sheria za nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uaminifu na kwa uwezo wangu wote kwa mujibu wa viapo nilivyoapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Jimbo la Ilala ili uwe Mbunge wao wa kipindi kingine cha miaka mitano. Naomba nikupongeze pia kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu na umahiri ulioonesha katika Bunge la Kumi na Mbili, ukiwa Naibu Spika katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge, ndiyo uliotupa imani sisi Wabunge kukuchagua kwa kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge pamoja na wananchi wa Tanzania kukutakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu ya kuongoza mhimili huu wa Bunge kwa mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuingia Bungeni.

Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu ya uwakilishi wa wananchi kupitia chombo hiki kitukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba kutoa hoja kwa mujibu wa kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanywa na Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 51 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge watakakumbuka Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba, mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile, ndani ya siku 14 baada ya kushika madaraka yake, Rais atamteua Mbunge wa kuchaguliwa kutoka jimbo la uchaguzi anayetokana na chama cha siasa chenye Wabunge wengi zaidi anayeelekea kuungwa mkono na Wabunge walio wengi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naye hatashika madaraka hayo mpaka kwanza uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa azimio litakaloungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoliarifu Bunge lako hili Tukufu, Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Dkt. Lameck Nchemba ni Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchguzi la Iramba Magharibi. Pili, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anatoka Chama cha Mapinduzi ambacho kwa mujibu wa matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 yaliyotangazwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ndicho chama chenye Wabunge wengi zaidi humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa mujibu wa masharti ya Ibara hiyo ya 51(2) ya Katiba, Mheshimiwa Rais amelileta jina la Mheshimiwa Dkt. Mwiguli Lameck Nchemba katika Bunge hili kwa ajili ya kuthibitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu makubwa ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ninaliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wake, yameainishwa katika Ibara ya 52 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nayo inatamka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 52 (1): "Waziri Mkuu atakuwa na madaraka ya juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania." *(Makofi)*

Ibara ndogo ya pili: "Waziri Mkuu atakuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni."

Ibara ndogo ya tatu: "Katika utekelezaji wa madaraka yake, Waziri Mkuu atatekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi Waziri Mkuu ni kiungo muhimu kati ya Bunge na Serikali. Kwa maneno mengine, yeye ni daraja muhimu kati ya wananchi na Serikali na ni Msaidizi Mkuu wa Rais katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ni majukumu mazito na makubwa ambayo ili kuyatekeleza yanahitaji mtu mchapakazi, mtu hodari, mtu anayejituma, mtu mwenye busara, mtu mwenye upeo mpana wa uelewa wa mambo na mtu aliye na uwezo wa kubeba majukumu mengi bila ya kutetereka. Madaraka hayo yanahitaji mtu makini katika kulinda na kutetea Katiba ya nchi, sheria, kanuni na taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amewasilisha jina la Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ili lithibitishwe na Bunge kwa sababu anafaa na ana sifa zote hizo nilizozitaja hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la uchapakazi, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba sio mgeni kwa

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia sio mgeni kwa wananchi kwa ujumla. Historia yake katika nyadhifa mbalimbali alizowahi kuwa nazo zinalithibitisha hili ninalolisema. Watu wengi ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaufahamu uwezo wake wa kufanya kazi kwa muda mrefu bila kujali saa za kawaida za kufanya kazi. Vilevile, wanaufahamu uwezo wake wa kujituma usiku na mchana bila ulalamishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwezo wake huu umejidhihirisha katika muda wote alioshika nyadhifa mbalimbali za uongozi wa umma ndani ya Serikali na katika Taifa kwa ujumla. Pamoja na nafasi nyingine alizoshika katika utumishi wa umma, nizitaje hizi kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba amewahi kushika nafasi mbalimbali katika Baraza la Mawaziri, zikiwemo nafasi ya Naibu Waziri wa Fedha na Mipango; aliwahi pia kuwa Waziri wa Kilimo; pia aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; aliwahi kuwa Waziri wa Katiba na Sheria; na wadhifa wake wa mwisho alikuwa Waziri wa Fedha, kazi ambayo ameifanya kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba tukiachana na nyadhifa hizo chache nilizozitaja miongoni mwa nyadhifa alizowahi kushika, ni mchumi mbobevu, mwenye Shahada ya Uchumi, mwenye Shahada ya Uzamivu *(Doctor of Philosophy)* katika masuala ya uchumi. Mtakubaliana na mimi kuwa kwa uzoefu na ubobevu huu wa kitaaluma, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ni mtu sahihi kwa nafasi hii ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ni mtu mwenye busara nyingi kama ilivyo kawaida kwa watu wa aina yake. Ni msikivu wa hali ya juu, anapokumbana na tatizo lolote anashaurika na hupokea ushauri kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ana uwezo wa kuchambua na kupima hoja

mbalimbali. Upeo wake mpana na uelewa wa mambo katika kufikia maamuzi, umejidhihirisha katika utumishi wake wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaziwasilisha sifa hizi kwenu ili sote kwa pamoja tumthibitishe Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba aweze kuyabeba majukumu yote yanayoendana na wadhifa wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani anaweza kuyahimili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyaeleza hayo yote, sasa kwa heshima na taadhima ninaliomba Bunge lako Tukufu lithibitishe uteuzi wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Iramba Magharibi uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili awe Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitisha Azimio la Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio lenyewe ni kama ifuatavyo na nitalisoma:-

**Azimio la Bunge la Kumthibitisha Waziri Mkuu chini ya Ibara ya 51 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 33 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Kwa kuwa, Ibara ya 51 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inaeleza kwamba kutakuwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakayeteuliwa na Rais kwa kufuata masharti ya Ibara hii, ambaye kabla ya kushika madaraka yake ataapa mbele ya Rais;

Na kwa kuwa, tarehe 31 Oktoba, 2025 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilimtangaza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mshindi wa Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika uchaguzi uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliapishwa tarehe 03

Novemba, 2025 na kushika madaraka ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na leo hii tarehe 13 Novemba, 2025 ni siku ya 10 tangu Rais aapishwe kushika madaraka ya Urais. Hivyo, muda huo ni ndani ya siku 14 zilizotakiwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; *(Makofi)*

Na kwa kuwa, Chama cha Mapinduzi kimepata Wabunge wengi zaidi kuliko Wabunge wa Vyama vingine vinavyowakilishwa Bungeni na hivyo Rais anayo haki ya kumteua Waziri Mkuu kutoka miongoni mwa Wabunge waliochaguliwa katika majimbo ya uchaguzi miongoni mwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi;

Na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais amekwishamwarifu Mheshimiwa Spika kwamba amemteua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Iramba Magharibi kupitia Chama cha Mapinduzi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Spika amekwishawasilisha jina hilo katika Bunge hili Tukufu;

Na kwa kuwa, Ibara ya 51 (2) inaeleza kwamba Waziri Mkuu aliyeteuliwa hatashika madaraka hayo mpaka uteuzi wake uwe umethibitishwa na Bunge kwa Azimio lililoungwa mkono na kura za Wabunge walio wengi;

Kwa hiyo basi, kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 51 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaazimia kama ifuatavyo:-

Kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Jimbo la Uchaguzi la Iramba Magharibi, na ambaye ameteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amethibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Kanuni ya 33 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa kwa mujibu wa taratibu zetu, nitatoa nafasi kwa Wabunge wachache waliokaa Bungeni kwa kipindi kirefu kusema mawili matatu kuhusu hoja hii. Mheshimiwa Lukuvi, jiandae Mheshimiwa Jenista, jiandae Mheshimiwa Malecela, jiandae Mheshimiwa Ado, jiandae Mheshimiwa Simbachawene. Dakika tatu tatu.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kabla ya yote, ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha leo katika siku hii yenye nuru kubwa na upendo iliyotuwezesha kukutana hapa na kufanya kazi hii muhimu kabisa ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha sisi Watanzania kufikia uchaguzi uliofanyika tarehe 29 na kukamilisha kwa amani na utulivu na kutuwezesha sisi Wabunge humu ndani kuweza kuchaguliwa na kuaminiwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, leo nimshukuru tena kwa kutimiza kazi nyingine ya Kikatiba ya kutuletea mwenzetu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ili tumthibitishe kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelezo mengi yametolewa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, na mimi ninayaunga mkono kwa sababu ninathibitisha yote aliyoyasema ni sahihi, na pengine ni kwa sababu ni mtu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale Wana-CCM wenzangu niwakumbushe mengine ambayo ninadhani Mwanasheria Mkuu

hakuyaandika. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba tumekuwa naye, ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa miaka mingi. Amekuwa Mjumbe wa Kamati Mkuu ya Chama cha Mapinduzi kwa muda mrefu, na amekuwa Mjumbe wa Sekretarieti yetu ya Chama, lakini amekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Ninawakumbusha Wana-CCM wenzangu kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakukosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu amesema hapa kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni Mchumi mbobezi. Ni kweli amesomea, lakini niwakumbushe tu, kabla hajajiunga na uongozi wa Chama na Ubunge, alitokea Benki Kuu, kuthibitisha kwamba Benki Kuu hawachukui watu hivi hivi tu, wanachukua watu wenye uwezo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu huyu ametoka Benki Kuu kabla hajajiunga na masuala haya ya siasa.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Lukuvi, malizia.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa sisi tuliokaa Bungeni muda mrefu, tunajua uvumilivu alionao Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa mema na mishale mingi aliyopigwa, lakini hajatetereka, hajatetereka. Mafanikio tunayoyaona ndani ya nchi hii, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametekeleza miradi mingi sana iliyotuletea mafanikio, na sisi Wabunge leo tunajivuna na tumechaguliwa kutokana na hayo, lakini mkusanya ushuru ni huyu aliyowezesha mafanikio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaunga mkono jambo hili na ningependa Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuliunge mkono kwa asilimia mia moja ili tumheshimishe Mheshimiwa Rais, lakini tumpe nguvu na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ili aanze kazi yake vizuri. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jenista, jiandae Mheshimiwa Malecela.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuifikia siku hii ya leo.

Pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu kwa ushindi mkubwa ambao ameupata katika uchaguzi wa mwaka huu, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze na wewe pia kwa kukalia Kiti hicho. Tunakupongeza sana na tuna imani kubwa na wewe utatuongoza ili kufanikisha ndoto na maono ambayo tunayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijaendelea ninaomba nitamke kwamba ninaunga mkono hoja ya uteuzi wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba niseme, sifa zilizosemwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni stahiki na ni sahihi kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kupata madaraka hayo na kuweza kusimamia nafasi hiyo kubwa ya uratibu ndani ya Serikali, ili tuweze kufanikiwa kuyafikia malengo, na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa hizo nyingine ambazo zimesemwa na Mwanasheria Mkuu, ninaomba niongeze sifa chache. Kwanza, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ni mtu wa maono. Anayo maono ya kujua Taifa letu linataka kwenda wapi? Pia, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba anajua vipaumbele vya nchi hii. Nini ambacho kinatakiwa kufanyika kwa sasa katika Taifa letu la Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninasema hivyo? Kwanza, muungaji mkono aliyetangulia ameeleza vizuri mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, hakika yasingeweza kupatikana kama tungekuwa na Waziri wa Fedha ambaye hakutekeleza vizuri majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu mapato ya ndani katika nchi yetu ya Tanzania kupitia *TRA* iliyokuwa chini ya Wizara ya Fedha, yameendelea kuongezeka na kusababisha mageuzi makubwa ya maendeleo katika nchi yetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Mheshimiwa Rais wetu ametueleleza kupitia Ilani ya Uchaguzi, lakini ndani ya siku 100 anayo maono yake na malengo yake ambayo yanakwenda kumgusa Mtanzania mpaka wa hali ya chini. Maono hayo yanamhitaji Waziri Mkuu kama Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, ili yaweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwa huduma hizo za afya, ujenzi wa uchumi, mabadiliko ya kimfumo ndani ya Serikali yetu, usimamizi wa Serikali, kwa sifa alizonazo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, niwahakikishia maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, yatakwenda kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ninaomba uniruhusu niwashawishi Wabunge na kuwahakikishia uwezo wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba katika nafasi hiyo, unatokana pia na kazi kubwa aliyoifanya, na akishirikiana na Mawaziri wengine na yeye akiwa miongoni mwa Mawaziri ambao wametengeneza Dira ya Taifa tutakayokwenda nayo mpaka mwaka 2050. Kwa hiyo, tunakwenda kupata Waziri Mkuu anayelitazama Taifa mpaka miaka ya 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba ninafahamu Dkt. Mwigulu Nchemba alikuwa ni miongoni mwa wajumbe walioandaa Ilani ya Uchaguzi ya 2025/2030. Tumepata, tumeletewa Waziri Mkuu ambaye alikuwa ni mmoja wa waandaaji wa Ilani, kwa hiyo anaifahamu ilani hiyo na atakwenda kuisimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dkt. Mwigulu Nchemba ni jasiri na msimamizi wa mambo. Anataka mambo yatokee, kwa hiyo, bila shaka tumuungeni mkono katika nafasi hii, tumepata chaguo sahihi na tutakweda kusimama naye kutekeleza majukumu yetu kwanza kama Wabunge, lakini tutakwedna kumsaidia Mheshimiwa Rais na Serikali kuyafikia malengo ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono azimio hili na ninamtakia kila la heri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba katika kazi yake hii mpya ya Uwaziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante Mhesimiwa Mama Malecela jiandae Mheshimiwa Ado.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kampeni nzito sana aliyoifanya akituongoza na sisi wengine. Ninampongeza na Makamu wa Rais. Ninakupongeza na wewe umetupatia dakika tatu, sitazungumza mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri Mkuu. Pia ninampongeza kwamba tangu alipochaguliwa mara ya kwanza kuwa Rais huwa anawaona sana Mawaziri wa Fedha. Kipindi cha kwanza alipoteua Makamu wake wa Rais, alimwona Waziri wa Fedha ambaye alikuwa ni Makamu wa Rais aliyestaafu kama sikosei Mheshimiwa Dkt. Mpango, alimtoa akiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo amemwona Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba aliyekuwa aliyekuwa Waziri wa Fedha wetu, aliyekuwa mwenzetu tuliyekaa naye hapa kwa muda. Ninamkumbuka akiwa Mbunge nikiwa nina maana *backbencher,* akiwa Naibu Waziri, akiwa Waziri katika Wizara mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, sifa hii hakuna mtu alizungumza. Sifa kubwa ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye sasa anaenda kuwa Waziri Mkuu wetu, anafikika. Waheshimiwa Wabunge mlioko humu ndani lazima niseme ukweli, kuna watu wakiwa Mawaziri wanakuwa wagumu kufikika. Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba amekuwa Naibu waziri, Waziri, Waziri wa Fedha mtu yeyote anamfikia wakati wowote pale alipoketi. Waziri Mkuu ajaye, huyu

hapa, nyumbani kwake ni nyumbani kwa kila mtu. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu hajui, lakini ameigusa mioyo yetu sana. Mimi nina uhakika wale tuliokaa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba tunamfahamu, nyie mliokuwa nje ambao mmeingia sasa mlikuwa mnamsikia ni kijana mzuri sana, ana upendo kwa wenzie, anakukaribisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kuongea kwa muda mrefu, lakini ninaomba niwashawishi Wabunge wenzangu tumepata Waziri Mkuu mzuri. Sisi tunamtaka Waziri Mkuu atakayetupokea pale mbele, ukienda akupatie nafasi. Wote mtakuwa mnataka hivyo. Yule pale ndiye mwenzetu atakayetupokea wakati wowote. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa unyenyekevu mkubwa, ametuletea Waziri Mkuu ambaye Wabunge wote tunamhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ado, jiandae Mheshimiwa Tauhida Gallos.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kukushukuru kwa kuniona na kunipatia fursa hii ingawa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge hili, hatuna Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini nina imani kwamba yale nitayoyasema yataungwa mkono na Wabunge wenzangu wote kutoka upande wa Walio Wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ninapenda kusema kwamba mimi Ado Shaibu Ado ninasimama kuunga mkono hoja ya pendekezo la uteuzi wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ingawa ni vigumu sana kusema kwa uhakika sifa zote ambazo zitakuwa zimemsukuma Mheshimiwa Rais kutuletea jina la Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, lakini ipo

sifa moja ambayo mimi nina uhakika nayo, na itakuwa ni sehemu ya sifa zilizomsukuma Mheshimiwa Rais. Ni ukweli kwamba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ni mtu mchapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwetu sisi tulio wachache tunapenda kusema bayana kwamba, tunamuunga mkono kama ishara ya kumkopesha imani tukiwa na uhakika kwamba atachapa kazi. Maeneo ya matarajio yetu ni mengi sana, lakini hatuna muda hapa. La kwanza, tuna imani kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba atasimamia vizuri Serikali katika usimamizi wa rasilimali za Taifa katika kuwaletea wananachi maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, tuna imani kwamba atasimamia maboresho ya demokrasia nchini Tanzania na kuipatia Katiba mpya hasa ikizingatiwa ukweli kwamba tasnia ya siasa na vyama vya siasa kwa ujumla wake vipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. La tatu, ni imani yetu kwamba, ataongoza mapambano ya kushughulikia changamoto za kiuchumi na za kijamii zinazowakabili Watanzania. Hatakuwa Waziri Mkuu wa ofisini muda wote, atakuwa Waziri Mkuu wa *field* kama ilivyokuwa desturi yake tuliyomzoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu kutoka upande wa walio wachache wameniomba niwasilishe ombi ingawa limesemwa katika sifa zake kwamba, milango yake iwe wazi, atupokee wakati wote kwa sababu katika Bunge hili sisi sote tumekula kiapo kimoja cha kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kwa pamoja tusaidie jitihada za kuwaletea wananchi wetu maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwa wanakandanda Ndg. Nchemba ni Mwanayanga mwenzangu. Lakini ni imani yangu kwamba pendekezo la uteuzi huu litakuwa linaleta faraja siyo kwa Wanayanga peke yao, lakini kwa Wanasimba na kwa Watanzania kwa ujumla, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tauhida, jiandae Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nichukue fursa hii kuunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Rais kutuletea Waziri Mkuu mahali hapa. Nishukuru kwa maono yanayoendelea kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwenyezi Mungu anaendelea kuweka nguvu na maono makubwa ndani yake ya kuweza kuliendesha Taifa hili, ili liweze kusonga mbele. Maono yake juu ya kiongozi mwenzetu ambaye kaenda kupata nafasi ya kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu, tunashukuru sisi kama Wabunge, amekuwa kwetu sio Waziri tu, bali amekuwa kaka pia.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusimama waliweza kusema mengi juu yake. Wamesema ni mtu ambaye anafikika, lakini kwa wale Wabunge wenzetu ambao mmeingia, siyo kufikikia tu, yeye amekuwa kaka, na mwepesi kwa kila Mbunge aliyekuwemo humu ndani. Ana sifa nyingi ambazo zimeweza kuelezewa, lakini kwetu sisi kwa umri wetu, lile la kuona tunapata heshima ya kipekee ni pale tunapomfikia kuweza kutatua matatizo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa mambo makubwa aliyoyafanya ya Kitaifa lakini tumeona namna mfumo wa bajeti ulivyokuwa ukienda ndani ya Taifa letu, pale tunapompatia mawazo yetu kuangalia wanyonge kwenda kugusa matatizo ya watu wanyonge, alikuwa mwepesi kuweza kuyatatua. Imani yetu kwake bado ni kubwa, tunaamini kwamba bado tupo na yeye na bado mwelekeo wake utaendelea kuwa kama alivyo na hataweza kubadilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumeambiwa tuseme, na wengi tumeshasema maneno mengi, tunampongeza, lakini pia tunaunga mkono kwa mambo ambayo ameweza kuyafanya ndani ya Taifa hili. Waliopata nafasi, wameweza kuelezea tangu ndani ya chama chetu, Chama cha Mapinduzi ameweza kufanya mambo makubwa, lakini ndani ya Wizara kwa muda wa vipindi vinne nilivyoweza kukaa ndani ya Bunge, ameweza kutumika, kufanya kazi vizuri kwa unyenyekevu, kwa kujishusha, lakini isitoshe ameweza kufanya kazi hata kwa Mbunge mmoja

mmoja pale tunapokuwa na shida ndani ya majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii ambayo nimeipata, kwa niaba ya wenzangu, tuendelee kumpongeza hususan Rais wetu kwa maono ambayo Mwenyezi Mungu ameweka ndani yake. Pia, tumpongeze na kumtakia kila la heri katika safari yake hii ambayo anaendelea nayo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa hayo machache. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Simbachawene.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ushindi mkubwa alioupata kwa 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuletea Waziri Mkuu Mteule, Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba ambaye azimio limesomwa hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili sisi Wabunge tuweze kumthibitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasimama hapa kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kuwaomba kwamba kwa kweli hatuna sababu ya kutokumthibitisha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kura zetu zote. Sifa zake zimeelezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini pia zimesemwa na wasemaji waliotangulia. Hakuna shaka juu ya usomi na ubobezi alionao Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Hakuna shaka juu ya uzoefu wa uongozi alionao kuanzia kwenye chama na kwenye Serikali, kwamba, ameshika Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha na Uchumi na baadaye Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ameshiriki katika uongozi wa Wizara ya Fedha katika mazingira magumu na

tata tukitoa kwenye *Covid 19*. Pia, tulikuwa na miradi mikubwa ya kimkakati ambayo hakuna hata mmoja uliosimama, yote imeendelea kutekelezwa kwa sababu alikuwa katika kutafuta fedha akimsaidia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni Waziri Mkuu wa kipindi hiki ambaye anastahili na mwenye sifa zote. Bunge hili 90% kama sikosei ni watu wenye umri chini ya miaka 50. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa uzoefu walionao wa kukaa humu Bungeni na uzoefu wa uongozi, atatuunganisha vizuri sisi wazee na vijana waliokuja. Maana moja kati ya majukumu yake ni kusimamia shughuli za Serikali humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nimalizie kusema sifa chache ninazozifahamu za Ndugu yangu Waziri Mkuu Mteule Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba. Unachokiona usoni kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, ndicho kilichopo moyoni mwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu yeyote akienda kwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anahisi kama anaenda kumwona mtu wa chini sana. Ni mtu wa kujishusha na mtu ambaye hajikwezi. Pia, moja kati ya sifa nyingine kubwa ambayo ninaamini imemsukuma sana Mheshimiwa Rais, ni uhodari wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tupo hapa Bungeni, sisi wengine muda mrefu tumewaona Mawaziri wa Fedha mbalimbali; Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba atashuka *Airport* kwenye ndege atakuja moja kwa moja Bungeni hapa, siyo kitu chepesi. Atatoka nje ya nchi, ataingia Dar es Salaam, atakuja Dodoma, atakuja Bungeni hapa hata kwa dakika 15 yupo tayari kuja Bungeni hapa kwa sababu anajua Bunge ndiyo chombo kinachowawakilisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme kwamba, ninawaomba sana wenzangu Waheshimiwa Wabunge ili tumjengee heshima Waziri Mkuu wetu anayekuja lazima tumpe kura zote za ndiyo. Ili

tujenge heshima kwa mamlaka iliyomteua, ni lazima tumpe kura zote za ndiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono Azimio la kuthibitisha Waziri Mkuu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Mbarawa.

**MHE. PROF. MNYAA MAKAME MBARAWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuongea machache kuhusu hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa na ushindi wa kishindo. Pia, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Nchimbi kwa heshima kubwa aliyopata kuwa Makamu wa Rais wa nchi yetu. Nami ninapenda nichangie hoja iliyoko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe ninamfahamu sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. Nina bahati sana kufanya kazi na Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha kama wanne katika maisha yangu au katika utumishi wangu wa Wizara, lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni Mheshimiwa wa kipekee. Nimemwambia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu zaidi ya mara mbili kwamba, wewe ni Waziri wa Fedha wa kipekee tofauti na Mawaziri wa Fedha wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu huyu anafanya maamuzi, *whether* ni jambo kubwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anafanya maamuzi. Baadhi ya watu wanachukua muda mrefu kufanya maamuzi, lakini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anafanya maamuzi. Leo hii Waheshimiwa Wabunge na leo hii tunaona miradi mingi mikubwa ya kimkakati inaendelea nchi hii kwa sababu ya usaidizi mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya kazi kubwa sana na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu katika kipindi chote, amekuwa na maono makubwa, amekuwa mtafutaji mkubwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutafuta fedha na amekuwa msimamizi mkubwa kwenye miradi mikubwa ya kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambao Waheshimiwa hawajui Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ni mtu mkweli, ni mtu mkweli na anasimamia haki. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu hapendi kumwonea mtu. Tumekuwa na *incidence* nyingi ambazo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu amesimama kidete kuwatetea watu wengine. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwa uteuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anapenda haki na Mungu amemjalia leo amekuwa Waziri Mkuu Mteule, tunaamini ataendelea kufanya kama alivyofanya huko zamani. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kumleta Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba hapa mbele yetu, huyu ni Waziri Mkuu ambaye atatuvusha katika kipindi hiki kwa sababu ana uwezo mkubwa, ana maono makubwa na anapenda kutenda haki, nami ninakushukuru sana na ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwa pamoja tuunge mkono Azimio lililopo mbele yetu, tuweze kutenda haki kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana Wabunge wazoefu waliokaa kipindi kirefu ndiyo taratibu za Kanuni zetu. Sasa, ninaomba Katibu tuangalie *quorum* tujue wajumbe wako wangapi ili tuwe na hesabu kamili.

Katibu, wataalam wako wahesabu watu pamoja na utaratibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa maelezo kuhusu utaratibu wa kuthibitisha

uteuzi wa Waziri Mkuu na kama ilivyobainishwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, zoezi hili linafanyika kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 51(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia Kanuni ya 33 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu unafanyika kupitia upigaji wa kura za siri. Hivyo, kila Mbunge atapewa karatasi ya kura yenye jina la Waziri Mkuu Mteule na atatakiwa kupiga Kura ya Ndiyo au Hapana kwa kuweka alama ya vema kwenye kisanduku husika mbele ya jina hilo. Kila Mbunge atapiga kura yake mahali alipoketi na baada ya hapo masanduku ya kura yataletwa hapa yakiwa wazi ili ninyi Waheshimiwa Wabunge kama wapigakura muweze kuyathibitisha kabla ya zoezi la kuhesabu kura muweze kuyathibitisha kabla ya zoezi la kuhesabu kura kufanyika, chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge pamoja na wawakilishi watakaoteuliwa na Spika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge, iwapo Waziri Mkuu Mteule atapata kura nyingi za ndiyo, atatangazwa kuwa amethibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, japo kwa mbali tunayo karatasi hii ya kupiga kura, ina picha ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ina visanduku viwili hapa, ndiyo au hapana. Ukipiga kura sehemu zote za ndiyo na hapana kura inakuwa imeharibika, kwa hiyo, hili ninaomba tulizingatie.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, ninaomba sasa uridhie tuendelee na zoezi la kugawa karatasi za kura na kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsante. Idadi tayari tunayo ni 371. Wenye karatasi za kupiga kura waanze kugawa karatasi.

Wenye masanduku onesheni Waheshimiwa Wabunge masanduku yako wazi.

*(Hapa Karatasi za Kupiga Kura ziligawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mmekusanya kura? Anzeni kukusanya kura!

Waheshimiwa Wabunge, ninamteua na kumtangaza Mheshimiwa Jacqueline Msongozi na Mheshimiwa Agnesta Lambert kwenda kushuhudia kuhesabu kura. Waheshimiwa Wabunge, kuna Mbunge yeyote ambaye hajapata karatasi ya kupigia kura? Waheshimiwa Wabunge, wote tumeshatumbukiza karatasi zetu? Mheshimiwa Jacqueline na Mheshimiwa Agnesta muambatane na kura hizo.

Katibu, endelea tu na utaratibu.

*(Hapa kura Zilihesabiwa)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Ado nimepata salamu zako, nimepata salamu zako ndani ya Bunge leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kila Mbunge anatakiwa awe na kitambulisho akiwa katika maeneo ya Bunge au kwenye kazi zake. Kuna utaratibu mpya ambao umeandaliwa na Ofisi ya Katibu, badala ya kuvaa vitambulisho vile vya kuning'inia kila Mbunge, atapewa *badge* ambayo itamtambua yeye kuwa ni Mbunge halali. *Badge* hii ipo kwenye benki zetu na pia ipo kwenye vyombo vyote ili kukutambua. Hata hapa watu wa usalama ukivaa *badge* hii hana haja ya kukuuliza kitambulisho. *(Makofi)*

Pamoja na hayo bado tutawapa vitambulisho ambavyo mtavitumia kwenye mambo yenu na shughuli za kawaida nje ya Bunge; lakini ukiwa Bungeni hii itakutosha kuthibitisha kuwa wewe ni Mbunge na una *access* ya kuingia maeneo yote ambayo utakuwa umeruhusiwa kwa mujibu wa Shughuli za Bunge.

Watumishi wa Bunge watapita, kila *badge* ina namba, atakupa *badge* atarekodi na namba yako, itafahamika sifuri sifuri fulani, tatu tatu fulani, nne nne fulani, tumeelewana jamani? *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaangalia teknolojia hii mpya ya *badge*; sisi ni binadamu, kuna kupoteza lakini ninajaribu kuangalia haka kapini huku nyuma, uhai wetu humu ni miaka mitano Bungeni, kila siku ninabadilisha nguo ninaweka kengine naweka kwenye nguo nyingine, wengine wanabadilisha mara tatu kwa siku. Sasa ninajiuliza kakipotea ama kakivunjika hii pini kuna utaratibu mwingine tutapewa kwamba tunaweza kupewa vingine au namna gani? Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, kwa sasa nitakushauri usipoteze hiyo *badge*. *(Kicheko/Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutangaza matokeo na kabla ya hapo, ninaomba kutoa taarifa kuwa matokeo haya yamethibitishwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kutoka kambi ya walio wengi na Mheshimiwa Agnesta Kaiza kutoka kambi ya walio wachache.

Mheshimiwa Spika, matokeo ni kama ifuatavyo: Idadi ya kura za hapana ni sifuri, kura zilizoharibika ni mbili na kura za ndiyo 369. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, hii inafanya idadi ya kura zote zilizopigwa kuwa 371. Hivyo, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba

amethibitishwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu kwa jumla ya kura 369. *(Makofi/ Vigelegele)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, karibu utoe shukurani na ukimaliza kaa kwenye kiti chako rasmi. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA - WAZIRI MKUU MTEULE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa ruzuku ya uhai na kutukutanisha katika Bunge la 13. Ninamshukuru Mungu vilevile kwa hatua hii ambayo tumetoka kuishuhudia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Watanzania. Ushindi huo ni uthibitisho wa imani kubwa Watanzania kwake pamoja na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miaka mitano Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejitambulisha kuwa ni Rais anayetaka matokeo ya haraka yanayotatua matatizo ya Watanzania. Amefanya hivyo wakati alipoapishwa kulikuwa na tatizo kubwa la umeme, aliweka jitihada kubwa za kukamilisha mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na kuachilia umeme ule ambao umemaliza kabisa tatizo la kukatikatika kwa umeme na kuipa nchi ziada ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alipoingia madarakani kulikuwa na tatizo la vifo vya akinamama wajawazito pamoja na watoto kutokana na upungufu wa hospitali na vituo vya afya. Katika kipindi kifupi amejenga zaidi ya hospitali 119 za wilaya, zaidi ya vituo vya afya 649 katika kata mbalimbali na zaidi ya zahanati 2,800 kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi kulikuwa na shida ya shule pamoja na madarasa na tulikuwa tukiona baadhi ya wanafunzi wakisomea chini ya miti. Katika kipindi kifupi amejenga shule mpya zaidi ya 2,700 za msingi na amejenga zaidi ya shule 1,300 za sekondari na madarasa zaidi ya 97,000.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, katika sekta nyingine ikiwemo kununua *CT-Scan* hospitali zote za mikoa, *MRI* kwenye hospitali zote za kanda pamoja na kununua mitambo ya kuchimbia maji kwenye kila mkoa na kila ukanda. Hiki ndicho kilichowafanya Watanzania wamchague kwa wingi na nimetaja tu kwa uchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani hii kubwa. Ninatambua imani hii si kubwa tu kwake bali ni dhamana kubwa kwa Watanzania kwa kunipendekeza katika Bunge lako Tukufu kushika nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua uzito wa majukumu haya pamoja na matarajio yake pamoja na matarajio ya Watanzania. Nitafanya kazi kwa bidiii, kwa uaminifu na jitihada kubwa kuweza kukidhi matarajio hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Watanzania kuwa Makamu wa Rais. Tuna imani na utendaji wake na tunaamini kwamba atamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuchaguliwa na kuaminiwa kuwa Rais wa Zanzibar. Ushindi wake ni ishara na uthibitisho wa kazi kubwa alizofanya za kuwaletea maendeleo Wazanzibari. Tunamtakia kila la kheri katika utumishi wake mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndugu yangu Mheshimiwa Hamza Johari kwani amekuwa kiungo muhimu na amekuwa akisaidia sana majukumu yanayohusu sheria kama *custodian* wa masuala ya sheria wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la Kumi na Tatu.

Ninatambua nia yako thabiti ya kulifanya Bunge la Kumi na Tatu kuwa Bunge la Watanzania. Ninaahidi kwa niaba ya Serikali tutatoa ushirikiano wa dhati kuweza kuhakikisha kwamba unatimiza malengo yako hayo ya kulifanya Bunge la Kumi na Tatu kuwa Bunge la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais Mstaafu kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Tutamkumbuka kwa unyenyekevu wake, kwa maono yake na usaidizi wake uliojaa utii. Mheshimiwa Dkt. Mpango amefanya kazi yake kwa uthabiti mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu Mstaafu kwa kazi kubwa aliyoifanya bila kuchoka ya ufuatiliaji wa miradi na ufuatiliaji wa shughuli za Serikali na pia kwa unyenyekevu wake, uadilifu wake na kazi kubwa ambayo amefanya kwa Taifa letu. Ninaamini kila Mtanzania anatambua jitihada alizofanya katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, niruhusu niseme ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa imani hii kubwa waliyofanya ya kuthibitisha jina langu, ahsanteni sana. Wamenipa faraja na wamenipa deni kwa imani hiyo kubwa mliyonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaahidi tutashirikiana nao, Serikali itashirikiana nao, itapokea maoni yao, itapokea hoja zao, tutawasikiliza na niseme tutawasikiliza bila ubaguzi hata walio wachache watakuwa na fursa sawa kwa sababu Bunge lako ni Bunge moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, niseme tu tuko na kazi kubwa mbele yetu. Ninatambua ukubwa wa kazi iliyo mbele yetu, kazi kubwa kwa nafasi niliyopewa, kazi kubwa ya Serikali na kazi kubwa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hivi majuzi ilitunga Dira mpya ya 2025 - 2050 na awamu ya pili ya Serikali ya Awamu ya Sita ndiyo itakuwa awamu ya kwanza ya kutekeleza dira mpya.

Mheshimiwa Spika, unatambua kwenye mbio za vijiti za kupokezana, mwanzishaji wa mbio hizo kipande cha kwanza asipokimbia kwa mbio ndefu, kwa *speed* kubwa, hata wale watakaokuwa wanampokea watakuwa tayari wamechelewa. Sasa Serikali ya Awamu ya Sita kwa awamu ya pili ndiyo inaanzisha utekelezaji wa Dira ya 2025 - 2050. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dira hiyo imebeba matarajio na matumaini makubwa ya Watanzania, dira hiyo imebeba matumaini makubwa ya vijana ambao ndio hasa walengwa wa dira hiyo. Tuna kazi kubwa ya kuanza vizuri kwenye utekelezaji wa dira hiyo huku tukimalizia viporo vilivyokuwa havikukamilika kwenye Dira ya 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua pia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambayo imejumuisha masuala yote ambayo ni kero kwa Watanzania katika maeneo mbalimbali na nilikuwa ninafuatilia hata kampeni za uchaguzi na Waheshimiwa Wabunge kila eneo walikuwa wakijaziliza yale ambayo yapo kwenye Ilani ambayo ni mahitaji ya Watanzania katika maeneo yenu.

Mheshimiwa Spika, Ilani hiyo imebeba matumaini makubwa ya Watanzania na hasa kwa kuzingatia kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejitambulisha kuwa ni Rais wa matokeo, Rais wa matokeo ya haraka na Rais anayetatua matatizo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ambayo amepokea vijiji vikiwa havijapata umeme, ndani ya muda mfupi alimalizia vijiji vyote vikapata umeme. Watanzania wanatarajia takribani vitongoji 28,000 ambavyo havijapata umeme sasa vikapate umeme. Hayo ni mambo makubwa ambayo yanasubiriwa na Watanzania katika kipindi hiki kinachofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Mheshimiwa Rais ametoa ahadi kupitia Ilani ya Uchaguzi kushughulikia tatizo la ajira kwa vijana kwa kutengeneza ajira zisizopungua 8,000,000 kwa ajili ya vijana wa Kitanzania. Hii ni kazi kubwa ambayo tutafanyia uratibu usimamizi kuweza kuhakikisha kwamba ndoto ya Mheshimiwa Rais ya Watanzania hawa vijana wetu kupata ajira inatimia. Tutaratibu mpango mkakati ndani ya Serikali na kushirikisha Sekta Binafsi kuweza kuhakikisha kwamba dira hiyo ya Mheshimiwa Rais ya kutengeneza ajira zisizopungua 8,000,000 inakwenda kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Tanzania kuwa nchi tajiri bado tuna asilimia isiyopungua nane ya Watanzania wanaoishi katika umasikini wa kupindukia. Tuna takribani 26% ya Watanzania wanaoishi kwenye umaskini wa kipato. Niwakumbushe Watanzania; mimi umaskini wa Watanzania sijausoma kwenye kitabu, nimeuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maisha yangu haya katika umri wangu huu miaka takribani 32 nimeishi katika maisha hayo ya umaskini. Nimeishi katika maisha ambayo kwa wale wanaokumbuka kule vijijini mama zetu, dada zetu wakivaa gauni huwa wanajifunga nguo kiunoni, ile nguo anayojifunga dada yangu, ile nguo anayojifunga shemeji yangu, ndiyo ilikuwa nguo yangu ya kujifunika. Kwa hiyo, kabla hajamaliza shughuli zake za kila siku, silali mpaka akalale ili nipate shuka ya kujifunika na asubuhi kabla hajaanza kazi lazima niamke ili ile nguo niliyojifunika ndiyo yeye iwe nguo ya kujifunga ili aweze kuanza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua mazingira ya kulala, unaenda kuchunga ukirudi nyumba nzima inavuja na utakapolala inabidi ujifunike ile ngozi ili matone yale yanayoendelea kuvuja angalau yatue kwenye ngozi; ninayatambua maisha hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua mnaenda kula pamoja na watoto wote rika mbalimbali mpo takribani 20 kwenye chungu kimoja cha mboga, sahani moja ya ugali; inabidi utangulize

kuanza kula ugali mwingine bila mboga kwa sababu ukisubiri mikono ya kwenye mboga iishe ndiyo na chakula kitakuwa kimeisha, ninayatambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatambua matatizo haya ya ajira ambayo Mheshimiwa Rais anayaongelea. Ninatambua maumivu ya kusoma kwa shida na ukasubiria ajira ukiwa umekosa, ninatambua dira hiyo ambayo Mheshimiwa Rais anataka awapatie vijana takribani 8,000,000 ajira; ninatambua maumivu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipomaliza chuo nimefanya kazi ya kubeba zege kwenye kiwanda cha matofali ili upate kipato cha siku na mke wangu akiwa anapika mama lishe na wakati mwingine wakati anawagawia wabeba zege wenzangu wengine walikuwa wanatoa maneno makali, ninatambua adha hiyo. Niwahakikishie Watanzania hasa wa mazingira ya chini watasikilizwa kwenye kila ofisi ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila aliye Mtanzania hii nchi ni yake, Watanzania wote watasikilizwa kwa nidhamu katika ofisi za umma. Watanzania watafikisha kero zao na watumishi wa umma watakwenda kwenye makazi kwenye maeneo ya Watanzania kutatua kero za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiondoa miaka 32 hiyo niliyoielezea, miaka takribani 18 maisha yangu yamekuwa yamezungukwa na wahitaji kuliko walioridhika, nikiwa na watoto takribani 100 ninaokaa nao, nina bweni la wasichana na wavulana hapa. Ninatambua mahitaji na uhitaji wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo, ninaamini yale yaliyo dira ya Mheshimiwa Rais katika kutatua kero za Watanzania niwahakikishie Watanzania nitasimamia kwa uadilifu, nitasimamia kwa jitihada na nitasimamia kwa kuhakikisha kwamba hayo yanatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kazi kubwa hiyo iliyoko mbele yetu niliyoisema, watumishi wa umma na Watanzania sote

tuwe tayari. Lazima twende kwa *gear* ya kupandia mlima, lazima twende kwa *gear* ya kupita kwenye bahari yenye mawimbi, lazima twende kwa *gear* ya kupita kwenye anga lenye mawingu, na ni lazima chombo kifike salama na watu wake wakiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa watumishi wa umma wavivu, wazembe, wala rushwa na wenye lugha mbaya kwa Watanzania tuwe tayari. Wavivu wote na wazembe wote ndani ya ofisi za umma, nitakuja na fyekeo na rato. Maono ya Mheshimiwa Rais, na ahadi ambazo Mheshimiwa Rais amewaahidi Watanzania lazima zitekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, nitoe rai kwa Watanzania wote, haya yote ambayo tunayaongea, yale yote yaliyoongelewa kwenye dira, yaliyoongelewa kwenye Ilani ya uchaguzi, tuliyo na matamanio nayo, yale yote yaliyo ahadi ya Mheshimiwa Rais pamoja na Makamu wa Rais, yale yote yaliyo ahadi zenu Waheshimiwa Wabunge, yatatimia tu kama tutaendelea kumtanguliza Mungu katika mambo yetu kama Taifa na kama Taifa letu litakuwa Taifa lenye amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yatatimia tu, kama tutaendelea kumtanguliza Mungu katika mambo yetu yote Taifa na kama Taifa lina hali ya amani. Bila amani, yote tunayoyatamani, yote tunayotarajia, yote tuliyoahidiwa, yote viongozi waliyowaahidi, yote yaliyopo kwenye dira, yote yaliyopo kwenye Ilani hayawezi kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Watanzania wote tuwe na wajibu wa kuhakikisha kwamba nchi yetu ni ya amani. Tumtangulize Mungu hata kwa yale tunayoona ni magumu ili tuweze kuhakikisha kwamba Mungu anatusaidia kupata ufumbuzi wake, kwa sababu kwake yote ni mepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kumalizia, niishukuru familia yangu wamesimama nami mara zote, mke wangu Neema pamoja na watoto, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Iramba, niwashukuru sana kwa sababu pasipo wao kunichagua nisingepata sifa leo ya

kupendekezwa kuwa Waziri Mkuu. Ahsanteni sana wana Iramba. Ahsanteni sana Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa mara nyingine, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Uchaguzi wa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu katika shughuli za kazi ya leo ratiba zetu zilikuwa ni hizo mbili na leo tunatakiwa tumthibitishe na aape Naibu Spika wetu. Basi ninachukua fursa hii kumwita aje mbele ajieleze. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo kabla hajaja Naibu Spika, kuna maelezo ya Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge wafanye rejea katika Ibara ya 86(2)(3) lakini pia kanuni ya 11 na 12 na Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 86(2) ya Katiba inaelekeza kuwa, uchaguzi wa Spika utafanyika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya au katika Kikao cha Kwanza cha Bunge mara baada ya nafasi ya Naibu Spika kuwa wazi. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 85(1) ya Katiba na Kanuni ya 11(4) uchaguzi wa Naibu Spika utaendeshwa kwa utaratibu ule ule unaotumika kumchagua Spika isipokuwa kwamba, Mbunge hawezi kushiriki uchaguzi wa Naibu Spika iwapo hajaapa kiapo cha uaminifu.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti ya Katiba niliyoainisha hapo juu, tarehe 4 Novemba, 2025 tulitoa tangazo Na. 14824(b) katika Gazeti la Serikali Toleo maalum Na. 11 kutangaza kuwa uchaguzi wa Naibu Spika utafanyika tarehe 13 Novemba, 2025 na kuanisha utaratibu utakaotumika kwenye uchaguzi huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, tulielekeza kwamba chama chochote cha siasa chenye uwakilishi Bungeni kinachokusudia kushiriki katika uchaguzi wa Naibu Spika wa Bunge, kiwasilishe jina la mgombea wa chama husika ofisini kwa Katibu wa Bunge Dodoma kabla ya saa kumi kamili jioni tarehe 12 Novemba, 2025 ambayo ndiyo siku ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufika saa 10.00 jioni ya tarehe 12 Novemba, 2025 nilikuwa nimepokea jina la Mheshimiwa Daniel Barani Sillo kutoka Chama Cha Mapinduzi, ambaye baada ya uchambuzi wa kina nimejiridhisha kuwa amekidhi vigezo na masharti kwa nafasi ya Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunaye mgombea mmoja tu, utaratibu utakaofuatwa ni kwamba, mgombea huyu atafika mbele yenu ili kujieleza kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza, kuulizwa na kujibu maswali kama yatakuwepo na kisha kuomba kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi hilo kukamilika kila Mbunge atapewa karatasi yenye jina la mgombea na atatakiwa kupiga kura ya ndiyo au hapana mbele ya jina hilo. Aidha, kura zitakuwa za siri ambapo kila Mbunge atapiga kura yake mahali alipoketi na baada ya hapo masanduku ya kura yataletwa hapa yakiwa wazi ili nyie Waheshimiwa Wabunge kama wapiga kura muweze kuyathibitisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Nyongeza ya Kwanza ya Kanuni za Kudumu za Bunge, iwapo mgombea huyu atapata kura nyingi za ndiyo atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa, ninaomba tuendelee na zoezi la mgombea kujieleza na kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mgombea Kiti karibu. Mheshimiwa mgombea utajieleza na tutakuuliza maswali matatu kama yapo. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL B. SILLO – MGOMBEA NAFASI YA NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niliyesimama mbele yenu naitwa Daniel Baran Sillo, ni Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kutoka Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na wote kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya njema kukutana leo katika Bunge letu Tukufu, Bunge hili la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukishukuru sana chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa heshima kubwa iliyonipa ya kuniteua kuwa mgombea wa nafasi ya Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Bunge hili la Kumi na Tatu, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Babati Vijijini ambao wamenipa heshima ya kuwa mwakilishi wao ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa uniruhusu nieleze nafasi chache ambazo nimewahi kushika ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Januari, 2021 hadi mwezi Machi, 2024 nimehudumu katika Bunge hili kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Kuanzia mwezi Aprili, 2023 hadi mwezi Machi, 2024 nimehudumu pia kama Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nikimsaidia Mheshimiwa Spika na Naibu Spika katika kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, nimepata pia fursa ya kuwa Mjumbe wa Kamati ya Uongozi ya Bunge. Pia nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge, lakini pia nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Nilipata pia heshima kuanzia mwezi Machi, 2024 kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nafasi ambayo nimehudumia hadi tarehe 3 Novemba, 2025.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba, nafasi ya Unaibu Spika imeelezwa katika Ibara ya 85(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, lakini majukumu ya Naibu Spika yameainishwa katika kanuni ya 6(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025. Jukumu kubwa la Naibu Spika ni kumsaidia Spika katika uendeshaji wa Bunge.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie, mkinipa kura za imani nitamsaidia Mheshimiwa Spika katika uendeshaji wa Bunge letu, lakini nikisimamia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini hasa nikisimamia kanuni zetu za Bunge ambazo ndiyo mwongozo wa kuongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule, Waheshimiwa Wabunge, nipo mbele yenu kwa heshima na taadhima nikiomba kura. Ninaombeni nipeni kura za imani ili nimsaidie Mheshimiwa Spika katika uendeshaji wa Bunge letu Tukufu na ninatambua kwamba tupo hapa kwa niaba ya wananchi. Nitasimamia mijadala mbalimbali na nikipewa fursa na Mheshimiwa fursa kwa ajili ya maslahi mapana ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mteule ninaomba kura yako na Waheshimiwa Wabunge ninaombeni kura zenu. Ahsanteni sana.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Maswali.

**WABUNGE FILANI:** Hakunaaa!

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mgombea kakae. *Quorum*!

Waheshimiwa Wabunge, *quorum* yetu imebaki vilevile 371, wahudumu leteni maboksi mbele na gaweni karatasi za kura.

*(Hapa Wabunge Waligawiwa Karatasi za Kupigia Kura)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza, tuwaombe radhi sana kwa hitilafu hii. Wale ambao hawajapata wanyooshe mikono juu.

Waheshimiwa, tunaanza kukusanya kura. Onesheni hayo ma-*box*.

Waheshimiwa Wabunge, wote tumepiga kura?

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mawakala watakaoenda kuwakilisha kwenye chumba cha kuhesabia kura ni Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Devotha Minja.

Kura zote zimekusanywa? Ma-*box* yote yamesharudi? Yote matatu yako hapo? Haya msimamizi, toa amri bwana waende. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwenye shughuli ya uzinduzi wa Bunge rasmi kesho na Mheshimiwa Rais itakuwa ni saa 9.00

mchana, kwenye jengo hili. Sasa ninamwomba *AG* atengue kanuni ya kuruhusu baadhi ya viongozi kuingia ndani kesho.

Mheshimiwa *AG*.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**MHE. HAMZA S. JOHARI - MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 177(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

KWA KUWA Ibara ya 91(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kanuni ya 34(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, inaweka masharti ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kulihutubia na kulifungua rasmi Bunge.

NA KWA KUWA Mheshimiwa Spika wa Bunge amewaalika viongozi mbalimbali kuja kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akilihutubia na kulifungua rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

NA KWA KUWA Kanuni ya 164 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 inaeleza kwamba, wageni wanaoruhusiwa kuingia Bungeni watakaa maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao na kwamba, inabidi Bunge litengue Kanuni hizi, ili kuruhusu viongozi maalumu walioalikwa na Mheshimiwa Spika kuja kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge.

KWA HIYO BASI kwa mujibu wa Kanuni ya 177 (1), ninaomba kutoa hoja ya kutenguliwa Kanuni ya 164 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, ili kuwaruhusu viongozi wafuatao waingie ndani ya ukumbi wa Bunge Siku ya Ijumaa, Tarehe 14 Novemba, 2025:-

(1) Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(2) Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

(3) Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;

(4) Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(5) Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar;

(6) Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Zanzibar; na

(7) Mheshimiwa Spika wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa. Sasa nitawahoji kuhusu hoja *ya Kutengua Kanuni za Bunge ili kuruhusu Viongozi Maalum walioalikwa na Mheshimiwa Spika Kusikiliza Hotuba ya Mheshimiwa Rais Kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge*. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki hivyo, Kanuni imetenguliwa.

Katibu.

## MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutangaza matokeo ya uchaguzi wa Naibu Spika. Matokeo haya yameshuhudiwa na wawakilishi wawili, wa kwanza ni Mheshimiwa Cecilia Paresso kutoka Kambi ya Wengi na Mheshimiwa Devotha Minja kutoka Kambi ya Walio Wachache. Matokeo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya kura zilizopigwa ni 371, kura zilizoharibika sifuri; kura za hapana sifuri; kura za ndiyo ni 371. Hivyo, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo amechaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ya kura 371. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Katibu, kiapo, kiapo.

**NDG. BARAKA LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## KIAPO CHA NAIBU SPIKA

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Mgombea, kiapo. *(Makofi/Vigelegele)*

1. Mhe. Daniel B. Sillo

*(Mbunge aliyetajwa hapo juu Aliapa Kiapo cha Naibu Spika)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Mheshimiwa Sillo, una maneno mawili, matatu ya kushukuru.

**MHE. DANIEL B. SILLO – NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru tena Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya muda huu, lakini niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa imani kubwa waliyoonesha. Ninaomba niahidi ushirikiano kwao na niombe sana ushirikiano wao katika kutimiza wajibu huu ambao nimekabidhiwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuahidi pia, ushirikiano na kukushauri kwa uadilifu mkubwa kwa manufaa ya Watanzania. Ahsanteni na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninashukuru kwa ushirikiano, kazi zote zilizopangwa leo zimekamilika. Ahsanteni sana kwa namna tulivyoendesha kikao leo, ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu.

Kuanzia Jumatatu kutakuwa na Semina. Wabunge mjiandae na semina hizo ambazo ni mafunzo *(orientation) ya* kuwasaidia na kuwakumbusha majukumu ya Bunge, Kanuni na mambo mbalimbali ya Kibunge.

Baada ya maneno hayo, ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 9.00 alasiri.

*(Saa 6.41 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 14 Novemba, 2025 Saa Tisa Alasiri)*